KWA JINA LA ALLÂH , MWINGI WA REHEMA, MWENYE KUREHEMU

25/= Ksh

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

Volume 14, Issue 4

25th Shawwâl 1432

23rd Sept, 2011

YALIYOMO

MASEEH AD-DAJJAAL 1 - 4

AL MASEEH AD-DAJJAAL

Na: Muhammad Saalih al-Munajjid (حفظه الله)

Kuna zaidi ya maoni 50 ya kitaalamu juu ya maana ya neno Maseeh. Wanasema yakwamba neno hili linatumika kumuhusu aliye Mkweli; yaani Eesa (عليه السلام) na kwa Mpotofu aliye Mrongo (ad-Dajjaal). Maseeh ndie Mkweli, 'Eesa ibn Maryam (عليه السلام). Maseeh wa uongofu, alieponya waliozaliwa vipofu, wenye mbalanga, na aliyehuisha wafu kwa idhni ya Allaah (سبحانه وتعالى). Maseeh wa kirongo (al-maseeh ad-Dajjaal) ni mrongo anaepoteza watu, Maseeh wa upotofu atakaewachochea watu kwa kutumia alama atakayopewa, kama kuleta mvua, kuipa uhai ardhi baada yakuwa imekufa na kutoa mimea na miujiza mingine.

Kwa hivyo Allaah (سبحانه وتعالى) ameumba Maseeh wawili, walio tafauti. Wanazuoni wanasema sababu ya Dajjaal kuitwa Maseeh, ni kwa sababu mojawapo ya macho yake ni mamsooh (yaani "limefutwa", limepigwa msasa au kuondoshwa-yaani atakuwa chongo au atakuwa na kasoro kwenye jicho moja). Au ilisemwa yakwamba ni kwa sababu atatazama na kusafiri kwenye kila sehemu ya ardhi (yamsah) kwa siku arubaini... Rai ya mwanzo ndio iliyo sawa zaidi kwa sababu ya yaliotajwa katika hadeethi iliyopokewa na **Muslim no.5221**- kutoka kwa Anas ibn Maalik aliyesema: "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *'Dajjaal atakuwa chongo (mamsooh) katika jicho moja, na baina*

(Endelea kwenye Ukurasa wa 2)

NENO LA BUSARA

Siku moja 'Umar Ibn al-Khattaab (رضي الله عنه) alimuona mtu mmoja akiburuta *Izaar* yake, akamwita na kumuuliza: "Wewe una heidh?" Yule mtu akasema: "*Yaa Ameerul Mu'mineen*! Kwani mwana-mume hupata heidh?" 'Umar akamjibu, "Basi ni kitu gani kilichokufanya uburute *Izaar* yako chini ya vifundo vya miguu yako?" Kisha akaamrisha kuletwe kisu, akaikunja sehemu ya chini ya *Izaar* ya yule mtu na akakata kilichozidi chini ya vifundo vya miguu."

Kisa hiki kimeelezwa na Kharshah bin Al-Hurr. Riwaya yenyewe imepatikana kwenye kitabu cha Waleed An-Nasr, "*Al-Isbaal Lighayer Al-Khulayaa', Uk. 18,* ambayo ameinasibisha na at-Twabaree. Imesimuliwa kwa mukhtasar na Ibn Abee Shaybah katika Musannaf yake (V.8, Uk.393) kwa isnaad iliyo swaheeh, kama alivyosema an-Nasr.

THE QUR'AN & SUNNAH HAJJ / 'UMRAH AGENCY

1432HIJRI/ 2011 C.E

Assalaamu 'Alaykum Warahmatullaahi Wabarakaatuh:
Tunafuraha kuwajulisha yakwamba Insha Allaah mwaka huu 1432 Hijri/ 2011, tumeanza Barnaamij ya kupeleka watu Hajj.

Mipangilio Ya Safari

- Kuondoka ni katika wiki ya mwisho ya mwezi wa Dhul Qa'dah
- Kurudi ni mwisho wa mwezi wa Dhul-Hijjah
- Safari itaanza Mombasa – Nairobi – Jeddah
- Kurudi ni Jeddah – Nairobi – Mombasa
- Gharama ya Safari (ikiwemo Hoteli, Usafiri na Chakula – mara 3 kwa siku tukiwa Mina kwa siku tano)
- Class "B" ni $3800 U.S Dollars / Class "C" ni $3200 U.S Dollars
- Amma mas'ala ya Chakula (Makka na Madinah) kila mtu ni juu yake
- Tutakuwa na Darsa juu ya mas'ala ya Hajj kabla ya kuondoka na tutakapokuwa Makkah
- Tutaandamana na Daktari wetu kutoka hapa Mombasa Insha Allaah

Kwa Maelezo Zaidi

Fika katika Maktaba ya QSS iliyoko ubavuni mwa Tajj Hotel (Duka la tatu baada ya Duka la vitabu vya Dini), au
Wasiliana nasi kwa kutuandikia barua Pepe kwa info@qssea.net, au
Tupigie simu nambari mojawapo ya hizi zifuatazo:
+254 723471820 au +254 721473181, au +254 700365253

(Endelea Kutoka Ukurasa wa 1)

ya macho yake itaandikwa 'kaafir' ...".

MAANA YA NENO DAJJAAL

Neno Dajjaal limechukuliwa kutoka katika msemo "Dajala al-ba'eer (alimpakapaka Ngamia)", ikimaanisha pale walipomueneza Ngamia mzima lami. Mzizi wa hili neno dajala maana yake ni kuchanganya. Neno dajala hutumika kumaanisha kutatiza mambo kwa kusudi na kutofahamika vyema na kuwa na maana nyingi, Dajjaal ni yule azugumzae kwa maneno yasiyo ya kawaida, anaesema urongo mwingi na kuwadanganya wengi. Neno "Dajjaal" likawa ni sifa anayopewa mtu mrongo, mwenye jicho moja, Maseeh mrongo. Dajjaal amestahiki jina hilo kwa sababu ataficha ukafiri wake kutokamana na watu kwa kuwadanganya, kuwapotosha na kuwatatiza.

MAELEZO KUHUSU ALIVYO DAJJAAL NA HADEETH ZILIZOPOKEWA KUMUHUSU YEYE

Dajjaal atakuwa ni mtu miongoni mwa watoto wa Aadam (عليه السلام). Atakuwa na sifa nyingi zilizoelezwa katika hadeeth kuwawezesha watu kumjua na kuwaonya kuhusu maovu yake. Kwahivyo atakapokuja, waumini watamjuwa na hawatapotezwa nae. Watazijuwa athari zake ambazo aliye Mkweli, Mtume (صلي الله عليه وسلم) ametueleza kumuhusu. Alama hizi zitampambanua yeye kutokamana na watu wengine, ili pasiwe na mtu atakaedanganywa nae isipokuwa wale walio wajinga, na ambao kuangamia kwao kushakadiriwa. Twamuomba Allaah atuhifadhi na atupe amani.

Miongoni mwa sifa hizo ni: Atakuwa ni kijana barobaro mwenye uso mwekundu, mfupi, mwenye nywele nyingi za kipilipili, komo kubwa, na kifua kipana, chongo au mwenye dosari (mamsooh) kwenye jicho la kulia. Jicho hilo halitokuwa ni lenye kujitokeza wala kuzama, na litakuwa kama zabibu inayo oleya. Jicho lake la kushoto litafunikwa na pande nene la nyama lenye kumea pambizoni mwa jicho lake. Imeandikwa baina ya macho yake "Kaa faa' raa (ك, ف. ر) **(K-F-R**)", kwa herufi za kiarabu zilizo mbalimbali au "Kaafir (كافر)", kwa herufi zilizoshikana. Haya yatasomwa na kila Muislamu, msomi na asiekuwa msomi. Sifa yake nyengine atakuwa tasa kwahiyo hatozaa watoto. Zifuatazo ni baadhi ya ahaadeeth zinazotaja sifa hizo. Ahaadeeth hizi zinajenga sehemu ya daleel kuhusu kutokea kwa Dajjaal: kutoka kwa Abdullaah ibn Umar (رضي الله عنه) aliyesema: "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Nilipokuwa nimelala, nilijiona nikifanya Twawaaf katika Ka'bah, nilipomuona mtu mweusi mwenye nywele zilizo nyooka, akiwa amesimama baina ya watu wengine wawili, na akiwa na maji yakimtiririka kutoka katika kichwa chake. Nikauliza: "Huyu ni nani?" Wakajibu: "Mwana wa Maryam." Kisha nikazunguka nikamwona mtu mwenye uso mwekundu, amejengeka mwili vizuri, na nywele koto, chongo jicho la kulia, jicho lake limefanana na zabibu inayo oleya. Nikauliza: "Huyu ni nani?" Wakajibu: "Huyu ni Dajjaal." Mtu afananaye mno naye (Dajjaal) ni Ibn Qatan."* [al-Bukhari, no.6508; ibn Qatan alikuwa ni mtu kutoka kabila la Banu Mustalaq kutoka Khuzaa'ah].

Vile vile imepokewa kutoka kwa Ibn Umar (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) aliwatajia watu Dajjaal na akasema: *"Allaah si jicho moja, lakini Maseeh mrongo (al-maseeh al-dajjaal) ni jicho moja, chongo au lenye kasoro kwenye jicho lake la kulia, na jicho lake kama zabibu inayo olea ..."* [al-Bukari no.3184].

Katika hadeeth ndefu iliyo pokewa na al-Nawwaas ibn Sam'aan (رضي الله عنه) yasema: "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alimtaja Dajjaal asubuhi moja. Mara nyingine alimueleza kama mtu duni na mara nyingine akamueleza kama mtu muhimu mpaka tukadhani kuwa yuko katika viguzo vya mitende..."

Mojawapo ya umbile la ad-Dajjaal alilolisifu ilikuwa ni: *"Atakuwa ni kijana barobaro akiwa na nywele za kipilipili mno, na jicho lake lenye kuolea. Ni kama kwamba anafanana na Abd al-Uzzah ibn Qatan."* [Muslim no.5228].

Imehadithiwa na Ubaadah ibn al-Saamit (رضي الله عنه) kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) amesema: "*Nimewaambia mengi kuhusu Dajjaal mpaka nikahofia kuwa hamtaelewa. Dajjaal atakuwa ni mtu mfupi, mwenye matege, akiwa na nywele za kipilipili. Atakuwa na jicho lake, lisilokuwa limezama wala kujitokeza. Ikiwa utatatizika kuhusu yeye, basi kumbuka kuwa Mola wenu si yule aliye na jicho moja."* [Abu Dawood, no.3763. swaheeh jamii asagheer no.2455].

Abu Hurayrah (رضي الله عنه) alisema: "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"....ama kuhusu Maseeh mrongo, akiwa na jicho moja, na komo pana la uso na kifua kipana sehemu ya juu na atakuwa na kijongo..."* [Ahmad, no.7564].

Hudhayfah (رضي الله عنه) alisema: Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Dajjaal atakuwa jicho moja, chongo au lenye kasoro kushoto, na nywele zilizo nyingi. Atakakuwa nazo pepo na jahanam, lakini jahanam yake itakuwa ni pepo, na pepo yake itakuwa jahanam."* [Muslim no.5222].

Kulingana na hadeeth ya Anas (رضي الله عنه), Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Hakuna Mtume aliyetumwa ila aliwaonya watu wake kuhusu mrongo mwenye jicho moja. Ana jicho moja, lakini Mola wenu si chongo, na baina ya macho yake itaandikwa 'kaafir'"* [al-Bukhari no. 6598].

Na kulingana na riwaya nyingine: *"Kitakachoandikwa baina ya macho yake itaandikwa 'kaa faa' raa'."* [Muslim no. 5219].

Kulingana na riwaya nyengine iliyopokewa na Hudhayfah*: "Hii itasomwa na kila Mu'min, aliye msomi au asiyekuwa ni msomi."* [Muslim, no.5223].

Kutokamana na maana ilio wazi nikuwa maadishi hayo yatakuwa haswa, na ukweli wakuwa wengine watayaona na wengine hawatayaona , na wasiojuwa kusoma watayasoma si

(Endelea Kwenye Ukurasa wa 3)

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

shida. “Hili ni kwa sababu Allaah (سبحانه وتعالى) huwafanya watu wakafahamu mambo baada ya kukitizama, kama Apendavyo na pindi Atakapo. Kwahivyo Mu’min ataliona hilo kwa utambuzi wake, hata kama si msomi, na kaafir hatoweza kuona hata akiwa msomi. Kwa kipimo hichohicho, Mu’min ataona kwa utambuzi wake ushahidi ambao kaafir hatouona. Allaah atamuwezesha Mu’min kuelewa hata kama si msomi, kwa sababu mambo ya wakati huo yatakuwa matukio yakiajabu.” [Fath al -Baari- ibn Hajar al-Asqalaani, 13/100)

Al-Nawawi alisema: “Rai ilio swaheeh kulingana na wale waliosoma mas’ala haya ni kuwa haya maandishi yachukuliwe kama jinsi yalivyo, yakuwa ni maandishi ya kihakika ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) atayaumba kama alama, mojawapo ya ushahidi ulio wazi yakwamba (Dajjaal) ni kaafir na mrongo, kuudhihirisha urongo wake. Allaah ataionyesha alama hii kwa kila Muislamu, msomi na asiekuwa msomi, na ataificha kwa kila aliemkadiria kuangamia au atakaye kumjaribu. Hakuna sababu kwanini jambo hili lisiwezekane.” [Sharh al-Nawawi li Swaheeh Muslim, 18/60]

Na sifa nyengine yake ilitajwa katika hadeeth ya Faatimah bint Qays (رضي الله عنها) katika kisa cha al-Jassaasah, katika kisa hicho Tameem al-Daari (رضي الله عنه) alisema: *“ Basi tukakimbilia kwa haraka kwenye nyumba ya ibada, ambapo tuliliona jitu kubwa hatujawahi kuliona maishani mwetu, likiwa limefungwa na nyororo nyingi ambazo hatujawahi kuziona.”* [Muslim no.5235].

‘Imraan ibn Husayn (رضي الله عنه) alisema: “Nilimsikia Mtume wa Allaah (صلي الله عليه وسلم) akisema: “Tangu alipoumbwa Aadam mpaka Kiyama kitakapoanza hapatakuwa na kiumbe kikubwa kuliko Dajjaal.”’ [Muslim, 5239].

Dajjaal hatakuwa na watoto (kizazi) kama ilivyoelezwa katika hadeeth ya Abu Sa’eed al-Khudri (رضي الله عنه) aliye eleza yaliotokea baina yake na Ibn Sayyaad aliemwambia yeye: “Hukumsikia Mtume (صلي الله عليه وسلم) akisema yakwamba hatakuwa hana watoto?...” Abu Sa’eed akasema, ‘nikasema ndio ...” [Muslim no. 5209].

Kutokana na yaliyonukuliwa hapo juu, twaweza kuona yakwamba baadhi zake zimetaja yakuwa jicho lake la kulia ndilo chongo la lenye kasoro, na baadhi zao zimetaja yakwamba ni jicho la kushoto. Na riwaya zote ni swaheeh. Baadhi ya wanazuoni wakatafuta njia za kuzipatanisha riwaya hizo. Al-Qaadi ‘Iyaad alisema: “Macho yote mawili ya Dajjaal yatakuwa na kasoro, kwa sababu riwaya zote ni swaheeh. Jicho lake la kulia ndilo litakalokuwa limechubuka (mamsooh) tena limefifia, halioni, kama ilivyonukuliwa kwenye hadeeth ya Ibn ’Umar. Na jicho lake la kushoto ndilo litakalokuwa limezibwa na ngozi nzito iliyokunjana, na pia litakuwa na kasoro.” Kwahivyo macho yake yote mawili, la kulia na kushoto, yatakuwa na kasoro; kila mojawapo litakuwa na chongo; yaani, litakuwa na kasoro,kwa sababu neno la kiarabu lililotumiwa ni **A’WAR,** ndilo lililotumiwa kueleza kila kitu chenye kasoro, na latumiwa haswa katika kueleza macho yakiwa yana ulemavu. Jicho moja litakuwa halioni na jengine litakuwa na kasoro katika kuona.” an-Nawawi alikubaliana na uafikiano huu uliotolewa na al-Qaadi ‘Iyaad na al-Qurtubi vivile akalipitisha hilo.

Atakapojitokezea Dajjal

Dajjaal atajitokeza kutoka upande wa Mashariki, kutoka Khurasaan, kutoka miongoni mwa Mayahudi wa Isfahaan. Kisha atasafiri katika ardhi nzima na hatouacha mji wowote ila atauingia, isipokuwa Makkah na Madeenah, ambapo hataweza kuingia kwa sababu Malaika watakuwa wakiilida miji hiyo. Kulingana na hadeeth ya Fatimah bint Qays (رضي الله عنها), Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema kuhusu Dajjaal: *“Atajitokeza kutoka upande wa bahari ya Syria au upande wa bahari ya Yemen... La, bali ni kutoka upande wa mashariki...” na akaashiria kwa kidole chake katika upande wa Mashariki.* [Muslim no.5228].

Abu Bakr al-Siddeeq (رضي الله عنه) alisema: “Mtume (صلي الله عليه وسلم) alitwaambia: *“Dajjaal atatokezea kutoka upande wa mashariki kutoka kwenye ardhi iitwayo Khurasaan.”* [Tirmidhi, no. 2163.-swaheeh al-Jaami al-Sagheer, no. 3398].

Anas (رضي الله عنه) alisema: “Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *‘Dajjaal atajitokeza kutoka miongoni mwa Mayahudi wa Isfahaan, na pamoja nae watakuwa Mayahudi alfu sabiini, wakiwa wamevaa mataji.’”* [Ahmad, no.12865].

SEHEMU AMBAZO DAJJAAL HATOINGIA

Imeharamishwa kwa Dajjaal kuingia Makkah au Madeenah atakapojitokeza mwisho wa wakati, kwa sababu ya hadeeth zilizotajwa kuhusiana na hilo. Ama kuhusu kwengine, atakuingia kote huko, moja baada ya kwengine. Katika hadeethi ya Faatimah bint Qays (رضي الله عنها) yasema: “(Atasema): *‘Karibuni hivi nitakuwa na ruhusa ya kujitokeza. Basi nitajitokeza kisha nisafiri katika kila sehemu ya ardhi kwa siku arubaini na sitouwacha mji wowote ila nitauuingia, ila Makkah na Madeenah, ambayo nitazuiwa kuiingia , kwa sababu kila nikijaribu kuiingia, patakuwa na Malaika alieutoa upanga wake katika mkono wake, akinizuia kuiingia. Katika kila mlango patakuwa na Malaika wakiilinda.’”* [Muslim no.5228]

Imehadithiwa pia kuwa Dajjaal hataingia msikiti wa Sinai, au Masjid al-Aqsaa (Daru salaam-Jerusalem). Junaadah ibn Umayyah al-Azdi alisema: ‘Nilikuja kwa mtu miongoni mwa Maswahaba wa Mtume (صلي الله عليه وسلم) nikamuuliza anisimulie hadeeth aliyoisikia kutoka kwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) kuhusu Dajjaal.’ Akitaja hadeethi na akasema. *‘’Atakaa miongoni mwenu kwa mda wa siku arubaini, wakati ambao atakwenda kila mahali (katika ardhi) isipokuwa Misikiti minne: Masjid al-Haraam (Makkah) Masjid an-Nabawi (Madeenah) msikiti wa Sinai na Masjid al-Aqsaa.’”* [Ahmad

(Continued from page 3)

no. 22572]

Wafuasi Wa Dajjaal

Wengi wa wafuasi wa Dajjaal watakuwa miogoni mwa Mayahudi, Mafarsi na Waturuki na mchanganyiko wa watu wengine, zaidi wakiwa mabedui na wanawake. Imepokewa na **Imaam Muslim no.5237-** Kutoka katika hadeeth ya Anas bin Maalik (رضي الله عنه) yakwamba Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Wafuasi wa Dajjaal miongoni mwa Mayahudi wa Isfahaan watakuwa na idadi ya alfu sabiini, wakiwa wamevaa nguo nzito, za mistari kulingana na riwaya iliyopokewa na Imaam Ahmad, "Elfu sabiini Mayahudi elfu sabiini wakiwa wamevaa mataji."* [hadeeth no. 12865].

Kulingana na hadeeth ya Abu Bakr (رضي الله عنه) iliyotangulia hapo juu. *"Atafuatwa na watu ambao nyuso zao zitakuwa kama ngao zilizong'arishwa."* [al-Tirmidhi, no.2136].

Ama kuhusu mabedui kumfuata Dajjaal, hii ni kwa sababu wengi wao ni wajinga. Na kuhusu wanawake, hii ni kwa sababu wao ni rahisi kuvutiwa, na kwa sababu wengi wao ni wajinga. Imehadithiwa kutoka kwa Ibn Umar (رضي الله عنه) yakwamba alisema Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Dajjaal atakuja katika kidimbwi hiki Marriqanaat- ni bonde lililoko Madeenah-na wengi watakaomfuata watakuwa ni wanawake, mpaka mtu aje kwa mamake mkewe, mamake, binti yake, dada yake, na shangazi yake, na awafunge imara kwa khofu yakuwa watatoka kumfuata Dajjaal."* [Ahmad no.5099]

Fitnah Ya Dajjaal

Fitnah ya Dajjaal ndiyo itakayokuwa fitnah kubwa zaidi kutokea tangu wakati Allaah (سبحانه وتعالى) alipomuumba Aadam mpaka kitakaposimama Kiyama. Hii itakuwa ni kwa sababu ya miujiza mikubwa ambayo Allaah (سبحانه وتعالى) atakayomuumba nayo, itakayoizubaisha watu na kuwastaajabisha. Imehadithiwa yakwamba atakuwa pamoja naye pepo na moto, lakini pepo yake itakuwa moto na moto wake utakuwa pepo. Atakuwa na mito ya maji na milima wa mkate. Ataamrisha mbingu kuleta mvua na itanyesha. Na ataamrisha ardhi itoe mimea na ardhi itafanya hivyo. Hazina za ardhi zitamfuata na atakwenda katika safari yake kwa kasi, kama mawingu yasukumwavyo na upepo. Na atafanya matendo mengine ya ujasiri wa ajabu. Yote hayo yametajwa katika hadeeth swaheeh. Imaam Muslim amehadithia katika swaheeh yake kuwa Hudhayfah (رضي الله عنه) alisema: "Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Dajjaal atakuwa na jicho moja (lionalo) chongo katika jicho lake la kushoto, na atakuwa na nywele nyingi. Atakuwa na pepo na moto pamoja naye, lakini pepo yake itakuwa moto na moto wake utakuwa pepo.'"* [Muslim no.5222].

Akapokea Hudhayfah (رضي الله عنه): "Mtume kuwa Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema: *"Najuwa atakachokuja nacho Dajjaal. Atakuwa na mito miwili yenye kwenda, mmoja utakuwa waonyesha wazi kuwa ni maji na mwengine utaonekana wazi kuwa ni moto uwakao kwa ukali. Yeyote miongoni mwenu atakayeona katika nyinyi hayo, basi na achague mto utakaokuwa kama moto, kisha afumbe macho yake na ainamishe kichwa chake anywe kutoka humo kwani yatakuwa maji ya kuburudisha."* [Muslim no.5223].

Katika hadeeth ya al-Nawwaas ibn Sam'aan kuhusu Dajjaal, kuwa Maswahaba walisema: *'Ewe Mtume wa Allaah, atakaa kwa muda gani katika Ardhi?' Akasema, "Kwa siku arubaini: siku moja kama mwaka, siku moja kama mwezi, siku moja kama wiki, na siku zilizo baki kama siku zenu." Wakasema, "atasafiri kwa kasi gani kwenye ardhi?' Akasema: 'kama mawingu yanayo sukumwa na upepo. Atawajilia baadhi ya watu na awaite, na watamuamini na waitikie mwito wake. Kisha ataamrisha mbingu kuleta mvua, na ardhi kuleta mimea, na Ng'ombe zao zitawarudia jioni wakiwa na nundu zilizo juu mno, na matiti yao yamejaa maziwa, na mbavu zao zimenyooka. Kisha atawajia watu wengine na atawaita, lakini watamkanusha. Basi atawawacha na watakumbwa na janga la ukame, na mali yao yote itawatoka mikononi mwao. Atapita katika magofu na atasema: "Toa hazina yako!'- na mali yatamfuata kama bumba la nyuki. Kisha atamwita kijana anayeng'ara kwa ujana wake, na atamkata kwa upanga vipande viwili. Kisha ataweka mapande hayo mawili mbali mbali umbali wa mlenga shabaha na alama yake. Kisha atamwiita, na kijana yule atamjia na huku akitabasamu, na uso wake uking'ara."* [Muslim, no.5228].

Al-Bukhari kutoka kwa Abu Sa'eed al -Khudri (رضي الله عنه) yakuwa mtu huyu atakaeuliwa na Dajjaal atakuwa ni mmojawapo wa watu bora sana, ambaye atamwendea Dajjaal kutoka katika Mji wa Mtume (صلي الله عليه وسلم) na atamwambia Dajjaal: *"Mimi nashuhudia kuwa wewe ni Dajjaal ambaye Mtume (صلي الله عليه وسلم) alituhadithia kukuhusu." Dajjaal atasema (kuwaambia watu): "Mwadhania nini-nikimuuwa mtu huyu kisha nikamrudisha katika uhai, mtakuwa na shaka?" Watasema, "LA." basi atamuuwa, kisha amrudishie uhai wake. Kisha yule Mu'min atasema: "Wallaahi sijakuwa na yakini zaidi kukuhusu wewe kuliko nilivyo leo." Dajjaal atataka kumuuwa lakini hataruhusiwa."* [al-Bukhari no.6599].

Kulinga na hadeeth ya Abi Umaamah al-Baahili (رضي الله عنه), Mtume (صلي الله عليه وسلم) alisema kumuhusu Dajjaal: *'Miongoni mwa Fitnah zake ni kuwa atasema kumwambia mbedui: 'Unadhania kuwa nikikufufulia wazazi wako utaniamini na kushuhudilia kuwa mimi ni mola wako?' Atasema: 'Ndio'. Basi mashetwani wawili wajitokeza kwake kwa sura za baba na mama yake wakisema: 'ewe mwanangu mfuate hakika yeye ni mola wako.'"* [Ibn Maajah no.4067 – Imeorodheshwa kuwa swaheeh na al - Albaani, swaheeh al- Jaami al-Sagheer no.7752].

ENDELEA KATIKA MAKALA YAJAYO